# MUNGU MWEMA

## KWA SABABU BWANA NI MWEMA, NA HURUMA ZAKE NI ZA MILELE

CLINT BYARS

**MUNGU MWEMA:** Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; Rehema zake ni za milele
na Clint Byars

Kimechapishwa USA
©2010 na Clint Byars

Clint Byars ndiye mchungaji mkuu wa kanisa la Forward

Kinapatikana kupitia huduma ya Forward.
Anwani za mawasiliano ni hizi zifuatazo:
Barua: Forward Ministries, 3500 Hwy 34 E, Suite 15, Sharpsburg, GA 30277
Barua Pepe: info@forward.church
Tovuti: www.clintbyars.com
Simu: 770-828-5826

Isipokuwa iwe imeelekezwa vinginezyo, nukuu ya Maandiko katika kitika
Kitabu hiki imetolewa katika Biblia Takatifu, NENO, BIBLICA-Africa, 2009.

**Yaliyomo:**


Maswali ya kutatanisha…………………………......3

Katika upendo hakuna hofu………………………..4

Mungu hana hasira na wewe………………………6

Mbona maovu?........................................................8

Mbona mitihani na majaribu?................................10

## Maswali ya kutatanisha

“Mungu ni mwema… kila wakatati!” Je, umewahi kusikia msemo huu, ama hata umewahi kuusema mwenyewe? Na huu nao, “Mungu anatawala?” Ama, “Mungu ana mpango, huwezi ukaouonaKwa sasa lakini mbeleni utelewa kwa nini Mungu alikubali ___________________,” na ujazena msiba uliokupata ama uliompata mtu umpendaye. Tamko linalojulikana sana kumhusu. Mungu pengine ni huu, “Kila kitu chatendeka kwa kusudi.” Umewahi kuambiwa hivyo? Je,Umewahi kuuliza kwamba, “Ikiwa Mungu anatawala, kwa nini maovu yatendeka?” Kawaida
yetu ni kutupilia mbali hayo mawazo kwa kueleza kwamba Mungu ni mwenye enzi,
kumaanisha anaweza fanya chochote atakacho.

Misemo hii na maswali haya ni baadhi ya mawazo yakuchanganyisha ambayo mtu atapashwaKumenyana nayo. Tunaposikia misemo kama hii, hasa tukiwa katika hali ya changamoto na vigumu,huwa twaonelea kwamba labda ufafanuzi wa Mungu wa mema ni tofauti na wetu. Twafunzwakuamini kwamba Mungu ni mwema lakini kwa njia fulani twafikiri kwamba tafsiri ya Mungu ya mema inajumuisha machungu, mateso,

hasara, msiba, majaribu, magonjwa, ukosefu wa haki,
na hukumu. Viongozi pamoja na waamini wanasema “Mungu anakupenda” lakini wanmwekaMungu mbali zaidi ya kueleweka kwetu kwa sababu hatuna majibu mazuri ya haya maswali magumu.

Kupitia misemo hii, Mungu anakuwa mtu ambaye hatuwezi husiana naye kikamilifu kwa sababu hatuna uhakika ya kujua ni nini anaenda kufanya. Tunajua twapaswa kumpenda lakini kwa kuwatuna hizi vizuizi njiani, ni vigumu sana tujitolee kikamilifu kwake. Wengi wetu tumekutana na watu ambao ndio wanatarajiwa wamwakilkishe Mungu, lakini walituhukumu tu na kutuhubiria makosa yetu.

Katika kijitabu hiki, naomba nikupatie habari njema na nikueleze ukweli kuhusu jinsi Mungu anavyokuona na anavyo husiana nawe. Utagundua kwamba Mungu hauhukumu ulimwengu wakati huu na misiba, wala hajaribu kukufunza kwa kuletea maumivu.

## Katika Upendo Hakuna Hofu

1 Yohana 4:18
“Katika upendo hakuna hofu. Lakini upendo ulio kamili huitupa nje hofu, kwa sababu hofu inahusika na adhabu. Kila mwenye hofu hakukamilika katika upendo.”

Je, unaelewa huo mstari? Ikiwa tunamwogopa Mungu, ni kwa sababu hatujashawishika kwamba Anatupenda. Mstari huo unasema kwamba “upendo ulio kamili huitupa nje hofu.” Katika 1 Yohana 4:16 twaambiwa kwamba Mungu ni Upendo. Kwa hivyo tunaweza sema kwamba Mungu huitupa nje hofu. Lakini ngoja, nadhani twafaa kummcha Mungu. Lakini hiyo haimaanishi uoga jinsi tunavyofikiria kumcha! Katika Luka 4:8, Yesu ananakili Kumbukumbu la Torati 6:13; Alisema kwamba twapaswa kumwabudu Mungu. Alibadilisha neno “Mche” akatumia neno “Mwabudu.” Nafikiri kwamba mwana wa Mungu anastahili zaidi kukalimani maandiko jinsi aonavyo sawa.

Ujumbe hadi hapa ni kwamba, kama unamwogopa Mungu ni kwa sababu unafikiri anaweza kukufanyia maovu. Ukweli ni kwamba Mungu hataki umwogope. Tumefanywa kuaminiKwamba

twafaa tumwogope Mungu kwa sababu tukikosea, atatuhukumu ama ataruhusu taabu maishani mwetu kutufunza. Watu wengi wanahubiri na kufikiri kwamba dhambi yako inakutenganisha na Mungu na ukitenda dhambi, unaanguka kutoka kwa neema na inabidi urudi kwa Mungu ukitubu na kuomba msamaha.

Kuna matatizo mawili na hiyo namna ya fikira. Kwanza, Yesu alilipa gharama ya dhambi yako,wewe huwezi kulipa gharama hiyo kwa sababu wewe si sadaka kamilifu ya dhambi. Dhambi yako ilisamehewa mara moja tu yakutosha milele kupitia kifo cha Yesu msalabani. Mungu hawezi kukuhukumu kwa dhambi yako kwa sababu ameshamhukumu Yesu kwa niaba yako.

Toba si tunapomrudia Mungu halafu anatusamehe, Yeye amekwisha kukusamehe. Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. Toba hasa inamaanisha kubadili fikra. Waebrania 10:14-18 hakuna tena dhabihu yoyote inayotolewa kwa ajili ya dhambi. Dhambi zako zilisamehewa katika mwili wa Yesu msalabani, na hazitahesabiwa kwako tena.

*Huu ndio ujumbe wakristo wanafaa kueleza watu.*

2 Wakorintho 5:19 Kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao. Naye ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho.

2 Wakorintho 5:20 Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Kristo, kana kwamba Mungu anawasihi kwa kupitia vinywa vyetu, nasi twawaomba sana ninyi kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu.

2 Wakorintho 5:21 Kwa maana Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye.

Toba si toleo lolote unalotoa kwa ajili ya dhambi yako ili usamehewe.Umesamehewa katika Yesu. Toba ni pale unapohisi msamaha ambao Mungu amekwisha kukusamehe kasha unabadilisha fikra zako kuhusu mambo ulikuwa unatenda ama unaamini.

Pia, Mungu alisema hakumbuki tena dhambi zako. Mradi umemruhusu Kristo akufanye mwenye haki, kwa kukubali kifo, mazishi na ufufuo wake Kristo, unapandikizwa katika Agano Jipya.

Yeremia 31:34 ni unabii kuhusu jinsi Agano Jipya ingekuwa, na ujumbe wake mkuu, ni kwamba Mungu hakumbuki dhambi zako tena milele.

Mungu anaona dhambi lakini ameshahukumu zako kwa Yesu kwa hivyo hazitafakari wala hahusiani nawe kulingana nazo. Dhambi bado huleta mauti kwa njia nyingi lakini Mungu anatuona kama wenye haki kuanzia wakati Roho wake alifanya makao ndani yetu. Mungu hawezi kaa mahali popote isiyokuwa patakatifu.

Sawa, najua unafikiria hivi, nafaa kukamilika ndipo nimkubali Yesu. LA! Huna wema wa kutosha, ndio maana Yesu alikuja. Yohana 3:17 inatuambia kwamba Yesu alikuja ulimwenguni kutuokoa wala sio kutuhukumu.

Warumi 8:1 inatuambia kuwa hakuna hukumu ya ahdabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu.

Unaweza tia kikomo hapa na useme, liwe liwalo, simwamini wala sitaki kumkubali Yesu. Nakusihi uendelee kusoma kwa sababu habari hii yaendelea tu kuwa bora. Ulimwengu haujamtambua Mungu jinsi alivyo, lakini wakati umefika wa kueleza mambo bayana. Mungu hatukasirikii… Anatupenda!

## Mungu hana hasira na wewe… Anakupenda

Sote tumesikia Zaburi 7:11, “Mungu ni mwamuzi mwenye haki, Mungu aghadhabikaye kila siku.” Ndivyo mambo yalivyokuwa katika Agano La Kale. Mungu ni mwenye haki na anadai haki. Mungu alijua hatuwezi kuwa wenye haki kivyetu, hivyo ikambidi atupatie haki bure ili aweze kuhusiana nasi kwa njia mpya. Yeremia 31:32 inatuambia kuwa hili Agano Jipya halifanani na Agano La Kale. Agano Jipya latubadilisha kutoka watumishi hadi kuwa wana. Agano Jipya lasema kuwa tu wenye haki kwa imani katika kazi ya Yesu, wala si kwa bidii zetu. Agano Jipya ilifanya amani kati ya Mungu na mwanadamu.

Isaya 53 ni unabii mzuri unaohusu mambo Masihi angepitia na kutekeleza msalabani kwa wote watakaomwamini. Isaya 54 inafafanua jinsi maisha yatakavyokuwa kati ya Mungu na mwanadamu baada ya Masihi kupitia kifo hichi.

Isaya 54:9 inalinganisha ahadi hii mpya na ahadi Mungu alimfanyia Noa kuwa maji kamwe hayatafunika dunia tena. Je unaamini Mungu atatimiza ahadi yake ya kutofunika dunia yote na maji? Basi ahadi hii mpya ni kama tu hiyo ahadi.

Isaya 54:9 inasema "Kwangu mimi hili (msalaba wa Kristo) ni kama siku za Noa, nilipoapa kuwa maji ya Noa kamwe hayatafunika tena dunia. Hivyo sasa nimeapa sitawakasirikia ninyi, kamwe sitawakemea tena."

Kukemea hapa inamaanisha kuhukumu. Mungu anaahidi kwamba kwa sababu ya matokeo ya msalaba wa Kristo, kamwe hatakukasirikia tena, wala hatakuadhibu. Yesu hakuja humu ulimwenguni kutuhukumu, bali alikuja kutuokoa.

*Je, utamruhusu Yesu akuokoe?*

Kinachohitajika ni kuamini kwamba Yesu alikuja ulimwenguni na alifufuka mautini, akishatimiza mahitaji yote ya haki na sasa amekufanya mwenye haki bure.

Wakristo wengine hufikiri kwamba hii ni kuwapa watu leseni ya kutenda dhambi. Hiyo yafunua tu fikra za kufuata sheria. Ni dhahiri kwamba si sawa kutenda dhambi. Dhambi huua, lakini habari njema ni kwamba dhambi haikutenganishi na Mungu kwa sababu imeshalipiwa. Yesu alichukua adhabu yako!

Yesu aliwaambia watu waende na wasitende dhambi tena lisije likawapata jambo mbaya zaidi. Dhambi ina matokeo yake mabaya, lakini si Mungu

anayekuhukumu kwa kutenda dhambi ukishafanyika haki kupitia damu ya Yesu.

Paulo alikabiliana na fikra aliposema, “Ni nini basi? Je, tutende dhambi kwa kuwa hatuko chini ya sheria bali chini ya neema? La hasha!” Warumi 6:15. Mradi umempokea Yesu, haupaswi tena kuwa na hofu ati Mumnu atakukasirikia ama kutaka kukuadhibu ama kukuhukumu. Mungu amekamilisha hoja ya dhambi na sasa anatamani tu uhusiano wa upendo, uliohuru mbali na matendo tunayohisi kutimiza.

Warumi 5:6, 8-11

“Kwa maana hata tulipokuwa dhaifu, wakati ulipowadia, Kristo alikufa kwa ajili yetu sisi wenye dhambi. Lakini Mungu anaudhihirisha upendo wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. Basi kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki kwa damu Yake, si zaidi sana tutaokolewa kutoka katika ghadhabu ya Mungu kwa Yeye! Kwa kuwa kama tulipokuwa adui wa Mungu tulipatanishwa naye kwa njia ya kifo cha Mwanawe, si zaidi sana tukiisha kupatanishwa, tutaokolewa kwa uzima Wake. Lakini zaidi ya hayo, pia tunafurahi katika Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa kupitia kwake tumepata upatanisho.”

## Mbona Maovu?

Kufikia hapa, umeshasikia injili. Ukiwa umefanya uamuzi wa kupokea dhabihu ya Kristo, tafadhali mwambie mtu na uanze kusoma biblia katika Agano Jipya.

Kama umerukia ukurasa huu, hautapoteza kwani kile ninachoenda kukuambia kinaweza kubadili milele jinsi unavyomwona Mungu. Yatupasa kuwa wazi kuhusu ukweli hata unapopinga mambo tunayoamini. Tunajitambua kutokana na mambo tunayoamini kumhusu Mungu, kwa hivyo tunaposoma mawazo ambayo hatukubaliani nayo, tunahisi kwamba tunalengwa binafsi.

Jua tu kwamba wewe ni mwenye haki mbele za Mungu kwa sababu ya damu ya Yesu pekee, na kwa sababu umeamini mambo yanayofaa. Kwa kweli, nawezasema kuwa wakristo wengi wanaamini mambo yasiyofaa kuhusu swali kwamba, "kama Mungu ni mwema, basi mbona…"

Tumekosea sana ulimwengu kwa kumwambia kwamba Mungu anahusika katika majanga, maharibifu, magonjwa, na aina yoyote ya machungu. Kwa kuwa sasa tuko sehemu hii ya msalaba, lazima tukumbuke yaliyomo katika agano jipya. Mungu aliahidi kwamba hatakasirika,

kwamba hatakukemea, kwamba hatakumbuka dhambi zako, na kwamba umefanyika mwenye haki.

*Kwa hivyo, ikiwa Mungu ni mwenye nguvu zote, mbona ulimwengu upo katika hali uliopo?*

Jibu inapatikana katika uumbaji. Katika Mwanzo 1:26, Mungu alipeana utawala na ulinzi juu ya ardhi kwa binadamu. Mungu yaani aliweka binadamu atawale ardhi. Ilimfaa Mungu kafanya hivyo ili tuwe na uhuru kamili wa kuamua. Tusingekuwa na utawala wote juu ya ulimwengu huu, basi hatungekuwa huru kweli.

Mjadala kuhusu jinsi gani tulivyo huru utabaki kuwa hoja kwa Wakalvini lakini kweli ni kwamba hapo mwanzo, Mungu alipatia binadamu mamlaka juu ya Ardhi hii na matukio tunayooona si mapenzi ya Mungu, bali ni yale binadamu ameruhusu. Ukitaka kuona mapenzi ya Mungu, angalia bustani kamilifu la Edeni, halafu tena angalia mbinuni… mambo yote katikati ni yale yanayotendwa na binadamu.

Unawezasema, lakini yeye ni Mungu, anawezafanya jambo bado. Angefanya hivyo, hatungekuwa huru tena. Mungu ameweka Roho wake ndani yetu na sasa anafanya mambo kupitia

sisi.Yesu alisema kwamba ulimwenguni tutapata dhiki lakini kwamba ameushinda ulimwengu. Je, unaishi katika ulimwengu ama unaishi katika Yesu?

Isaya 54:15 inatuambia kwamba baada ya msalaba, mashambulizi yatakuja lakini haitatoka kwa Mungu. Makampuni ya bima yanakosea, majanga si matendo ya Mungu.

## Mbona Mitihani na Majaribu?

Kufika sasa pengine umefurahi kwamba Mungu hana hasira nawe, ama unahasira nami kwa kusema kwamba Mungu ana furaha. Wengi wenu watakubali kwamba Mungu hahukumu kwa hasira wala kusababisha mitetemeko ya dunia, lakini huenda bado unaamini kwamba Mungu anaruhusu mitihani na majaribu kutufunza na kutufanya jinsi atakavyo.

Yakobo 1 hutumika sana kusema kwamba Mungu huleta mitihani na majaribu kwetu ili tufindishwe. Zaidi ya kwamba wazo hilo linamfanya Mungu awe kama mdhalimu, linaacha sehemu muhimu.

Wengi hunukuu Yakobo 1:2 na 1:12, inayosema kwamba majaribu huleta taji la uzima, lakini mstari

wa 13 huachwa. Mstari wa 13 unasema, "Mtu anapojaribiwa asiseme, "Ninajaribiwa na Mungu" kwa maana Mungu hawezi kujaribiwa na maovu wala yeye hamjaribu mtu yeyote."

Neno "jaribiwa" hapa ina maanisha: mtihani ama jaribio. Ina maana kwamba Mungu hatutengenezei majaribu. Upendo hauhitaji hayo. Ni wema wa Mungu ndio unaotuelekeza kwenye toba, sio majaribu.

Sawa, lakini tusemeje kuhusu 1 Wakorintho 10:13 unaosema kwamba Mungu hataruhusu tujaribiwe kupita tunavyoweza? Isome maakini, haisemi kwamba Mungu ndiye anajaribu, inasema tu kwamba Yeye atatupa njia ya kutokea majaribu yanapokuja.

Nini basi kuhusu 1 Peter 1:7 inayotuambia tufurahi imani yetu inapojaribiwa? Tena, majaribu yaja, lakini hayatoki kwa Mungu. Hatufai kuweka mapitio yetu katika maandiko ili kufanya Bibilia iwe shambamba na mabo tunayoamini. Inatufaa kusoma Biblia na kuiamini. Si kwamba tuangalie hali ngumu halafu tuseme kwamba Mungu ameiruhusu kututia nguvu… hiyo si maandiko.

Tunajifunza katika mambo magumu, lakini mambo hayo sio mpango wa Mungu. Kwamba twajifunza

katika mabumu na twamsonga karibu na Mungu katika nyakati za dhiki haimanishi kwamba Mungu ndiye anazilete. Ukweli ni kwamba hatutaki kuwajibika kwa hali ya maisha yetu. Twaona heri kumlaumu Mungu, shetani ama mtu mwingine.

Nakusihi utafute agano jipya leo na umtambue Mungu mwenye upendo na Roho Mtakatifu mwenye nguvu. Yesu alifanya amani katikati yako na Mungu. Kubali zawadi yake ya utakatifu leo kwa kuamini tu katika kifo, kaburi na ufufuo wake kwa mkono wa Mungu.

Kama anaamua kukubali kazi Yesu alikufanyia kwa kifo chake, kaburi na ufufuo wake kama msimamo wako wa haki mbele za Mungu na hujui la kufanya, itambue tu na ueleze mwingine.

Yeyote aitaye jina la Yesu ataokolewa, hakuna mtindo wa kufuatilia, hakuna ombi la kiganga, ni uamuzi tu unaofanya moyoni mwako.

Wasiliana nasi kama tunaweza kukusaidia kwa njia yoyote.

www.clintbyars.com

www.forward.church